
# Komba

ISSN 0856 Toleo la 21 Jarida la Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania 2012


*Katika toleo hili...*




06 *Zijue Kanuni zitakazofanikisha utekelezaji wa MKUHUMI+*



13 *Kilimo Hifadhi*



17 *Mradi wa Haki.*



22 *Usimamizi shirikishi wa misitu*

# "Huwezi kudai haki bila kujua Haki"

**Uzoefu kutoka Mkutano Mkuu wa 11 wa MJUMITA**

***Na: Fatma Kitine, Mratibu kanda ya Mashariki***

Mnamo tarehe 16 mpaka tarehe 17 Novemba 2011, Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania MJUMITA ulifanya warsha ya siku mbili iliyofuatiwa na Mkutano Mkuu wa MJUMITA uliofanyika tarehe 18, mwezi wa 11 mwaka 2011. Warsha hii ilihudhuriwa na wadau mbalimbali wa sekta ya misitu wakiwemo wanamtandao wa MJUMITA kutoka kanda zote sita yaani kanda ya Mashariki, Magharibi, Kati, Kaskazini, Nyanda za Juu Kusini pamoja na Kanda ya Kusini. Wadau wengine ni pamoja na asasi zisizo za kiserikali kama vile TFCG, MEMP, Care International, Haki Ardhi na Mpingo Conservation. Wengine ni watumishi wa Serikali kama vile mwakilishi kutoka wakala wa misitu (TFS), maafisa misitu wilaya, mkuu wa wilaya ya kilosa, waandishi wa habari pamoja na mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mh; Joel Nkaya Bendera ambaye ndiye aliyekuwa mgeni rasmi.

> "Haki katika Misitu kwa manufaa ya jamii na wadau wote"

Haki ni mojawapo ya kitu muhimu sana ambacho kila mwanajamii anastahili kukipata hata hivyo inawezekana mwanajamii asitendewe haki na hivyo kulazimika kudai haki hizo za msingi, ,lakini swali la kujiuliza ni kwamba utadai vipi haki kama hufahamu haki?

Mada hii ilielezwa kwa undani na Mkurugenzi wa TFCG Bw. Charles Meshack ambaye aliwapa maswali washiriki na baadae kufafanua kwa undani zaidi kwa wanawarsha juu ya haki za wanavijiji katika kudhibiti ardhi zao. Bw Meshack alisisisitiza kuwa wanajamii wanayo haki ya kutoa maamuzi yoyote yanayohusiana na misitu iliyopo kwenye ardhi zao kupitia mkutano mkuu wa kijiji, endapo kutakuwa na mamlaka zingine kama halmashauri za wilaya zikafanya maamuzi katika utolewaji wa vibali basi maamuzi haya ni lazima yaizinishwe na serikali ya kijiji

*Inaendelea Uk.3*



## Kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji

Kuanzia mwezi februari mwaka 2011, MJUMITA kupitia mradi wa Haki katika Misitu umekuwa ukifuatilia masuala mbalimbali ya utawala bora katika sekta ya misitu katika maeneo mbalimbali nchini kwa kushirikiana na wanamtandao na waandishi wa habari wa vyombo mbalimbali.

Toleo hili namba 21 la komba linaelezea zaidi matokeo ya hatua mbali mbali zilizochukuliwa na wanamitandao, mradi wa Haki katika Misitu , serekali na wadau mbali mbali katika kuhakikisha utawala bora katika sekta ya misitu nchini unaboreshwa. Sehemu kubwa ya matokeo haya yametokana na kazi kubwa ambayo imefanywa na Mradi wa Haki katika misitu kwa kushirikiana na wanamitandao na serikali kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita na kazi hizi ziliripotiwa vizuri katika toleo namba 19 la jarida la Komba.

Mradi unapenda kushukuru ushirikiano ambao tumekuwa tukipata kutoka kwa wanamitandao, maafisa misitu, wakurugenzi wa wilaya na maafisa wengine katika kufanikisha malengo yake. Aidha kwa namna ya kipekee kabisa mradi unapenda kutoa shukrani kwa mtendaji mkuu wa wakala wa misitu nchini, Bwana Juma Mgoo ambae amekuwa akishiriki kwa vitendo kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi wanaoshirikiana na serekali katika kusimamia misitu nchini.

Mwisho ninatoa wito kwa wanamitandao kuendelea kuibua na kutoa taarifa za mapungufu ya utawala bora na uhalifu katika misitu ya jirani na maeneo yao. Taarifa hizi watoe kwa viongozi wa halmashauri za wilaya au katika namba zetu za simu za kila kanda na sisi tutawasaidia kuzifikisha kwa wahusika. Aidha nitoe wito kwa watumishi wa serekali kushirikiana kwa karibu zaidi na wananchi na kuzifanyia kazi kwa wakati changamoto wanazokumbana nazo katika usimamizi wa misitu katika maeneo yao. Misitu haiwezi kusimamiwa na wataalamu peke yake wala na wananchi peke yake bali kwa kushirikiana kwa pamoja na kila mmoja kuona anawajibika kuhakikisha kuwa misitu yetu inahifadhiwa vizuri.
Asanteni sana na nawatakia usomaji mwema.

**Rahima Njaidi**
**Mkurugenzi Mtendaji – MJUMITA**



# Tahariri

Wapendwa wasomaji wa Jarida la Komba, ni mara nyingine tena tunakutana katika safu hii ya kubadilishana mawazo ya masuala mbali mbali yaliyojiri katika harakati za kupambana na kukabiliana mabadiiko ya tabia nchi.
Uharibifu wa misitu umekuwa tatizo la dunia na changamoto kwa mataifa mengi hususan yanayoendelea. Athari zake haziishii kwa mazingira naviumbe hai pia huchangia kwa kiasi kukubwa mabadiliko ya tabia nchi. Matukio ya ukataji wa miti hovyo na uharibifu wa misitu yanaendelea kutokana na msukumo wa hali ya mahitaji ya maendeleo mijini.

Pamoja na juhudi zinazoendelea katika kukabiliana na suala hili, MJUMITA na wanachama wake wameona ushirikiano wa baadhi ya viongozi katika ngazi za wilaya ukiongezeka kadri siku zinavyoendelea.

Toleo hili limetoa habari mbalimbali za MJUMITA na wadau wake kuhusiana na masuala ya utekelezaji wa shughuli za mradi wa "Haki kwa misitu" na mradi wa MKUHUMI kwa ajili ya jamii na uhifadhi wa misitu Tanzania. Mradi huu unalenga kubooresha utawala bora katika sekta ya misitu na kuongeza uwajibikaji ili wananchi na jamii kwa ujumla inufaike na rasilimali za misitu wakati huohuo kutekeleza sera na sheria za misitu.

Kutokana na changamoto za usimamizi wa misitu katika maeneo mbalimbali, mradi huu umekuwa mstari wa mbele kushirikiana na wadau wote kuhakikisha kuwa haki inatendeka na rasilimali za misitu zinanusuriwa. Hii itadhihirishwa kutokana na habari mbalimbali kutoka kanda za MJUMITA.

Tunawatakia usomaji mwema,
**Bettie Luwuge | Mhariri**

*inaendelea kutoka Uk. I*

na endapo kuna lolote litakaloenda kinyume basi wanajamii watalazimika kuripoti kwa waziri wa ardhi ambaye ndio atatoa tamko la mwisho kuhusiana na madai yao.

Bwana Meshack alieleza pia juu ya haki za kijiji endapo kijiji hakina haki milki ya ardhi na kufafanua wazi kwamba hakuna ulazima wa kuwepo kwa mpango wa matumizi bora ya ardhi pamoja na hati milki ya ardhi ndipo eneo lijulikane kama ardhi ya kijiji.

Alielezea pia juu ya mipango ya usimamizi wa misitu ya wilaya na kueleza bayana kwamba hakuna uhusiano kati ya mipango hii na misitu iliyopo ndani ya ardhi ya kijiji, lakini endapo kamati ya uvunaji itakaa kikao kuzungumzia juu ya masuala ya uvunaji katika ardhi ya kijiji ni vyema ikawashirikisha mwenyekiti pamoja na afisa mtendaji wa kijiji husika.

Alifafanua pia kuwa njia pekee ya kuboresha misitu ni kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi pamoja na kuanzisha misitu ya vijiji na kuwaeleza wanawarsha kwa makini juu ya umuhimu wa kuanzisha hifadhi za kijiji ambazo zitawawezesha wanajamii kusimamamia misitu yao kwa urahisi zaidi.

Bw. Meshack alifafanua pia juu ya maeneo yasiyoruhusiwa kuvunwa na kuainisha maeneo yaliyo ndani mita sitini baada ya vyanzo vya maji, maeneo yenye miinuko mikali pamoja na maeneo ya misitu ya hifadhi yaliyo chini ya serikali kuu kama maeneo yasiyostahili kuvunwa.

Hadi mwisho wa mada wanajamii walionekana kuelewa kwa undani juu ya haki zao kama wadau waishio pembezoni mwa misitu. Hivyo basi ni vyema jamii hizi zikachukulia kwa makini mada hii ili kuhakikisha zinapata haki zao za msingi kama wadau wa Msitu kwa kutumia Mradi wa Haki katika Misitu. Ni vyema wanaMJUMITA wakaelewa wazi kwamba mradi huu unawapa fursa ya kipekee kuripoti matukio mbalimbali hususani yale yaliyo kinyume na utawala bora ambayo huwapelekea kukosa haki zao. Hili litawezekana tu endapo wanajamii watakuwa mstari wa mbele kuripoti matukio mbalimbali yanayokwenda kinyume na sera na sheria za misitu katika ofisi za kanda husika. Ikumbukwe wazi kwamba kauli mbiu ya mkutano wa mwaka jana ni "HAKI KATIKA MISITU KWA MANUFAA YA JAMII NA WADAU WOTE"